Written by Administrator
Monday, 03 December 2012 10:07 - Last Updated Monday, 03 December 2012 10:50

VIEWED {hits}260{/hits} TIMES 

Kikosi cha Mabingwa wa Kombe la Vilabu Bingwa Afrika Mashariki na Kati kombe la KAGAME timu Young Africans Sports Club,  leo kimeendelea na mazoezi ikiwa ni wiki ya pili katika uwanja wa shule ya Sekondari Loyola kujiandaa na maandalizi ya mzunguko wa pili wa Ligi Kuu ya Vodacom na Kombe la Kagame mwakani mwezi Januari 2013.     Young Africans ambayo mpaka sasa inaongoza msimamo wa Ligi Kuu ya Vodacom kwa kujikusanyia pointi 29, imeshuka dimabani mara 13, ikishinda michezo 9, sare michezo miwili (2) na kufungwa michezo miwili. Kocha Mkuu Ernie Brandts amesema wameamua kuanza mazoezi mapema ili kujiandaa vizuri na mzunguko wa pili wa pili Ligi Kuu unaotazamiwa kuanza Januari 26, 2013 kwa Young Africans kucheza na timu ya Prisons ya Mbeya katika Uwanja wa Taifa jijini Dar es salaam.

Aidha kocha Brandts pia amesema huu ni wakati mzuri wa kujiandaa na mashidano ya kombe la Kagame ambalo linatazamiwa kufanyika mwakani mwezi Janruai pia nchini Rwanda japokuwa bado haijathibitshw arasmi.

Uongozi wa klabu ya Young Africans umefkia hatua ya kuiepelea timu kambi nchini Uturuki mara baada ya sikukuu ya X-mass na itakaa huko kwa kipindi cha wiki mbili, kisha kurejea nchini na kucheza michezo ya kirafiki kabla ya kuanza kwa mashindano.

**Wachezaji waliofanya mazoezi leo ni:**
**Walinda mlango**
: Yaw Berko, Ally Mustapha 'Barthez', Said Mohamed,

**Walinzi:**
Stephano Mwasika, Godfrey Taita,  Oscar Joshua, Mbuyu Twite, Ladislaus Mbogo, Ibrahim Job,Juma Abdul,

**Viungo:**
Nizar Khalfani, Omega Seme, Nurdin Bakari, Shamte Ally, Idrisa Rashid, David Luhende

**Washambuliaji:**
Didier Kavumbagu, Said Bahanunzi, Jeryson Tegete